**OFISI YA MKUU WA MKOA WA PWANI**

# HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI MHESHIMIWA ENG. EVARIST NDIKILO WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO CHA WADAU WA ZAO LA UFUTA MKOA WA PWANI

**TAREHE 27 MEI, 2020**

- ***Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa,***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,***
- ***Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Pwani (CORECU),***
- ***Mkurugenzi wa Soko la bidhaa Tanzania (TMX),***
- ***Mkurugenzi wa Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania,***
- ***Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya,***
- ***Wakuu wa Idara,***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

Asalaam Aleikum, Bwana Yesu asifiwe.

**Ndugu Wadau,**

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kukutana siku hii ya leo tukiwa na afya njema. Pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kufika kwenu katika kikao hiki cha wadau wa zao la ufuta katika Mkoa wetu.

Vile vile napenda kuwapongeza Ndugu zetu Waislam kwa kufanikisha Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kufanya sherehe za Iddi kwa amani, utulivu na upendo.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha washiriki wote katika kikao hiki cha kujadili maandalizi ya msimu wa ununuzi wa ufuta kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani unaotarajia kuanza mwishoni mwa mwezi Mei 2020.

**Ndugu Wadau,**

Lengo la kikao hiki ni kujadiliana namna ya kufanikisha maandalizi ya msimu wa ununuzi wa ufuta kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani ambapo minada inatarajiwa kuanza kufanyika mwishoni mwa mwezi Juni 2020. Tofauti na minada tuliyozoea kwenye zao la Korosho, minada ya Ufuta itafanyika kwa njia ya kielectroniki kupitia Soko la Bidhaa Tanzania (Tanzania Mercantile Exchange - TMX).

Hivyo, katika kikao cha leo tutapata nafasi ya kupitia taarifa ya Mkoa, Mwongozo wa ukusanyaji na uuzaji wa zao la ufuta Ufuta kwa msimu wa 2020/2021, taarifa ya hali ya maandalizi ya ununuzi wa Ufuta na taarifa ya TMX kuhusu uendeshaji wa minada kwa njia ya kieletroniki. Vile vile

tutapata nafasi ya kujadili changamoto zilizojitokeza katika msimu uliopita na kuweka mikakati ya utatuzi wake.

**Ndugu Wadau,**

Mkoa wa Pwani ni miongoni mwa Mikoa inayozalisha zao la Ufuta kwa wingi nchini. Katika msimu wa mwaka 2019/2020, jumla ya kilo 7,326,980 za Ufuta zenye thamani ya Shilingi 19,352,727,619.13 zilikusanywa na kuuzwa kupitia maghala ya AMCOS. Matarajio ya Uzalishaji wa zao la ufuta kwa msimu wa mavuno wa mwaka 2020/2021 unakadiriwa kuwa tani 13,250 zitakazokusanywa kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi 53.
Ni wazi kuwa zao hili ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wetu wa Pwani. Hivyo wajibu wetu kama Serikali ya Mkoa ni kuhakikisha Zao hili linamnufaisha Mkulima kukuza uchumi wa Mkoa wetu.

**Ndugu Wadau,**

Mkoa unatambua Changamoto zilizojitokeza kwa msimu wa ununuzi wa mwaka 2019/2020 kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi ikiwa ni pamoja na:-

1. Wakulima kufanya udanganyifu kwa kuchanganya ufuta na vitu vingine hususani mchanga,
2. Baadhi ya Viongozi wa AMCOS kutokuwa waaminifu kwa kufanya udanganyifu kuhusu kiasi halisi cha ufuta kilichokusanywa tofauti na kile kilicholipiwa na wanunuzi,

3. Ubora duni wa miundombinu ya maghala pamoja na ucheleweshaji wa zoezi la usafirishaji ufuta kutoka kwenye maghala kutokana na umbali na ubovu wa miundombinu ya barabara.

Changamoto hizi zilipelekea wadau kulalamikia ufanisi mdogo wa mfumo huu mzima wa ununuzi wa zao la ufuta kwa msimu uliopita.

Ili kukabiliana na changamoto hizo Serikali imeamua kuanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani kuanzia msimu wa mwaka 2020/2021. Kupitia mfumo wanachama na wakulima watapeleka Ufuta kwenye maghala ya Vyama vya Ushirika vya Msingi ambavyo vitapeleka Ufuta kwenye Maghala Makuu yaliyosajiliwa na Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania. Maghala Makuu yatapeleka taarifa za Ufuta uliopokelewa kwenda TMX ambayo itaratibu minada.

**Ndugu Wadau,**

Nimeambiwa kuwa Mfumo huu umeleta ufanisi mkubwa kwa zao la Ufuta kwa msimu wa 2019/20120 katika baadhi ya maeneo Nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa Mkoani Dodoma. Hivyo basi, matarajio yetu ni kwamba mfumo huu utatatua changamoto zilizojitokeza katika Mkoa wetu kwa msimu uliopita na hatimaye wakulima kupata bei nzuri.

Aidha, ili mfumo wa stakabadhi ghalani uwanufaishe wakulima, natoa maelekezo yafutayo:-

1. Zao la ufuta liendelee kununuliwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani ili wakulima wapate bei nzuri.

2. Mnada wa Ufuta uratibiwe na TMX kwa kushirikiana na Wadau wote Muhimu wa zao hili.
3. Mara baada ya mnada kufanyika malipo yafanyike kwa haraka kwa wakulima na Wanunuzi wajitahidi kutoa mzigo haraka kwenye maghala ili kutoa nafasi kwa mzigo mwingine unaofuata**.**
4. Wakulima waongeze uzalishaji na ubora wa zao la Ufuta kwa kuweka mashamba yao katika hali ya usafi na kuepuka kufanya udanganyifu kwa kuchanganya Ufuta na vitu vingine kama mchanga.
5. Wakulima wote walipwe kupitia Akaunti zao, hivyo tukawahimize kufungua Akaunti.
6. Wakala wa Vipimo wasimamie ubora wa mizani ili kuzuia wakulima kupunjwa kiwango cha mazao yao.
7. Viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika wahakikishe vifungashio (viroba) vya ufuta ghafi vinapatikana kwa wakati kwa wakulima.

**Ndugu wadau,**

Napenda kusisitiza kuwa sote tufuatilie kwa makini na kuchangia mada zitakazowasilishwa kadri iwezekanavyo ili tupate uelewa mpana utakaotusaidia kutekeleza vizuri majukumu yetu ya kusimamia mfumo huu wa stakabadhi ghalani kwa zao la ufuta.

Baada ya kusema hayo natamka kuwa kikao cha wadau wa zao la ufuta nimekifungua rasmi na ninawaruhusu kuendelea na majadiliano kwa kuzingatia tahadhari dhidi ya ugonjwa wa *COVID-19*.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**